# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA PILI

**30 OKTOBA, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 30 OKTOBA, 2024

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI WAZIRI MKUU:**

**20. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza kiwango cha Pensheni kwa Wastaafu nchini.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**21. MHESHIMIWA UMMY ALLY MWALIMU (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Mgandini katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.

**22. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Zahanati ya Isagehe Kahama itapandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya.

**23. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza miundombinu na Vifaa Tiba katika Hospitali ya Mji Tarime kutokana na kuelemewa na Wagonjwa kutoka maeneo ya jirani.

**24. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Shule za Msingi katika Vijiji vya Kalundi, Lyapinda na Londokazi Nkasi kusini.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**25. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi ya TAKUKURU Wilayani Kakonko.

## OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

**26. MHESHIMIWA ASK. JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kila Awamu inatekeleza Maono ya Dira ya Taifa 2050.

## WIZARA YA NISHATI:

**27. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia Wananchi na Makampuni 18 ya Viwandani na Zegereni Mji wa Kibaha waliopitiwa na umeme wa KVA 400.

**28. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha upatikanaji wa huduma ya Gesi kwa matumizi ya Magari na Mitambo nchini.

**WIZARA YA KILIMO:**

**29. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Miradi ya Umwagiliaji itaanza kutekelezwa katika Jimbo la Mlalo.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**30. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Minara ya Mawasiliano ya TBC - Lushoto.

**WIZARA YA MAJI:**

**31. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatoa Tsh. 300,000,000/= kwa ajili ya Mradi wa Maji Kijiji cha Igunga kutoka chanzo cha Ntomoko.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**32. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Mwananchi aliyekamilisha maombi ya Kitambulisho cha NIDA anaweza kupatiwa ndani ya muda gani.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**33. MHESHIMIWA JUSTIN LAZARO NYAMOGA (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Mitambo ya Kuchakata Sukari inayotengenezwa na TEMDO itafungwa katika Kata ya Mahenge – Kilolo.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**34. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, nini mkakati wa Serikali kufanya DRC kuwa na Bandari nyingine zaidi ya iliyopo ya Kalemie.

**WIZARA YA UJENZI:**

**35. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini kipande cha Barabara ya Turiani - Mziha hadi Handeni kitajengwa kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**36. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini wizi wa Mifugo utadhibitiwa Wilaya ya Rorya.

**WIZARA YA AFYA:**

**37. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imechukua hatua gani za kuimarisha Tiba za Kitalii kutokana na kuimarika kwa huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **30 OKTOBA, 2024** | **KATIBU WA BUNGE** |